



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA NYANG’HWALE**



**TAARIFA KWA UMMA**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyang’hwale anawatangazia Wananchi wote kuwa H/W Nyang’hwale imetoa Jumla ya **Tsh. 465,850,410.07** kupitia mapato ya ndani kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali kama ifuatavyo;

Kiasi cha **Tsh. 6,843,000** kwa ajili ya Ujenzi wa Kichomea taka Zahanati ya Lushimba.

Kiasi cha **Tsh. 18,000,000** kwa ajili ya ukamilishaji wa matundu 12 ya vyoo vya wasichana Shule ya Sekondari Kafita.

Kiasi cha **Tsh. 30,000,000** kwa ajili ya ukamilishaji wa matundu 10 ya vyoo Shule ya Msingi Albert Mnali na matundu 10 Shule ya Msingi Bululu

Kiasi cha **Tsh. 151,139,050** kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma 10 ya vyumba vya madarasa katika Shule za Msingi (Shibalanga 02, Nyashilanga 02, Bumanda 01, Nyang’hwale B 02, Izunya 01, Lyulu 01 na Lushimba 01).

Kiasi cha **Tsh. 149,868,360.07** kwa ajili ya ukamilishaji wa Zahanati za Vijiji vya Kabiga, Nyang’hwale, Kasubuya, Kanegele, Bugombela na Kaboha

Kiasi cha **Tsh. 90,000,000** kwa ajili ya mikopo ya asilimia 10 kwa Vijana, Wanawake na Watu wenye ulemavu.

Kiasi cha **Tsh. 20,000,000** kwa ajili ya shughuli za Lishe.

**Imetolewa na,**  
**Kitengo Cha Mawasiliano Serikalini,**  
**Halmashauri ya Wilaya ya Nyang’hwale.**

**Agosti 17, 2024**

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Nyang’hwale, S.L.P 352, Geita  
Barua pepe: [ded@nyanghwaledc.go.tz](mailto:ded@nyanghwaledc.go.tz)